

**HALMASHAURI YA WILAYA YA MPWAPWA**  
**TAARIFA YA UTEKELEZAJI, KAMATI YA HUDUMA YA**  
**UCHUMI**

KATIKA KIPINDI CHA ROBO YA PILI (OKTOBA-DESEMBA)

---

**Mhe, Mwenyekiti,**

Kamati ya uchumi inajumuisha idara tano nazo ni idara ya mifugo na uvuvi, idara ya Kilimo, Umwagiliaji na Ushirika, Idara ya ujenzi, idara ya ardhi pamoja na idara ya Usafi na mazingira.

**Mhe, Mwenyekiti,**

Kamati ya uchumi ilikaa kikao chake mnamo tarehe 25.01.2018 na kisha kuazimia yafuatayo;

- Afisa Ushirika asimamie SACCOSS zilizopo kwa zile ambazo zinaweza kufufuliwa zifufuliwe tena ili kuweza kuwasaidia wananchi.
- Afisa ushirika afwatilie kwa kina SACOSS ya Malolo ili kuweza kujiridhisha kuwa ni aina gani ya mkopo ulitolewa kwa wanachama, ni vyema ikajulikana kama wanachama walikopeshwa mbolea au fedha taslimu.
- Ili kupata uwakika wa heka 45 za shamba ambalo awali lilijulikana kuwa ni mali ya SACOSS ya Matomondo ni vyema sehemu iliyobaki baada ya kuharibiwa na mvua (korongo) ikapimwa kwa uhakika zaidi.
- Elimu juu ya mazao ya biashara (Parachichi, vitunguu swaumu, tangawizi na iliki) katika maeneo ya kanda za juu Mpwapwa itolewe kwa wingi ili kama wanapenda kuanza kulima basi waweze kuanza kulima badala ya kutegemea fedha ambazo zimetengwa kwenye bajeti peke yake.

**Mhe, Mwenyekiti,**

- Napenda kulitaarifu Baraza lako tukufu kuwa kamati ya huduma ya Uchumi haijakubaliana na kutolewa kwa hati kwa ndugu Sigfrid Ishengoma pamoja na ndugu Anna Mashauri na

Philipo Mashauri. Hatua ya utoaji Hati imekataliwa na hata majengo aliyoongeza ndugu Sigfrid Ishengoma ambayo zipo katika eneo la Hospitali hayatambuliki kwani umiliki wake bado ni wa serikali hatua hii pia ifanyike kwa upande Anna Mashauri na Philipo Mashauri waliongeza ujenzi nje ya makubalioano katika eneo la Ujenzi.

- Kamati pia imeshauri kuwa wale wote ambao waliuziwa nyumba za serikali wasiziendeleze kwa kuzingatia masharti ya awali waliopewa pindi walipouziwa nyumba hizo.
- Afisa ardhi awasilishe majibu ya mgogoro wa ardhi katika kijiji cha Kisima na Mtera.
- katika kufanikisha suala la uzoaji taka mjini ni vyema wananchi wakashirikishwa na ikiwa mwananchi atatakiwa kulipishwa kiasi cha fedha basi apatiwe risiti.
- Katika kikao kijacho kutolewe taarifa juu ya kuondolewa kwa taka zilizokusanywa katika eneo la kwa Karoli.
- Idara ya Ardhi ijiridhishe na majengo (miradi) yote iliyoanzishwa na wananchi na kuelezea hatua iliyofikiwa za ujenzi.

### **Mhe, Mwenyekiti**

Naomba Baraza lako tukufu liweze kuridhia mapaendekezo na maazimio yaliyofikiwa na kamati hii,

Nawasilisha.

.....

Mhe. Richard .E. Maponda

**MWENYEKITI KAMATI YA UCHUMI**

**HALMASHAURI YA MPWAPWA**